



UJUMBE MUHIMU KWA WAKIMBIZI NA WATAFUTA HIFADHI WOTE WANAOSHI MJINI KUHUSU VIRUSI VYA CORONA (COVID-19)

Mnamo tarehe 15 Machi 2020 serikali ya Kenya ilitangaza hatua maalum za kuzuia kueneza zaidi virusi vya corona (COVID-19). Kutoka tarehe 27 Machi 2020, **kuna amri ya kutotoka majumbani kati ya saa moja jioni mpaka saa kumi na moja asubuhi**. Hairuhusiwi kutoka nyumbani mwako wakati huu, au utakamatwa na polisi.

Zaidi ya hayo, mnamo tarehe 6 Aprili 2020, serikali ya Kenya ilitangaza kuwa **hakutakuwa na harakati yoyote ndani au nje ya eneo la jiji la Nairobi kutoka tarehe 6 Aprili 2020 na kaunti za Kilifi, Kwale na Mombasa kutoka tarehe 8 Aprili 2020**. Usijaribu kuingia ndani au nje ya maeneo haya au utakamatwa na polisi. Unaweza kuendelea na harakati zako ndani ya eneo unaloishi, You can continue to move within the area where you are living, lakini hakikisha umevaa vifuniko vya uso wakati uko katika maeneo yako na umati wa watu.

Kwa watu wanaoishi katika eneo la jiji la Nairobi, hii inahusisha Kaunti ya jiji la Nairobi, Sehemu ya kaunti ya Kiambu hadi daraja la mto Chania (Thika), pamoja na Rironi, Ndenderu, Jiji la Kiambu; Sehemu ya kaunti ya Machakos hadi Athi-River, pamoja na Katani; Sehemu ya kaunti ya Kajjido pamoja na Kitengela, Kiserian, Ongata Rongai na jiji la Ngong.

Tafadhali usizunguke sana wakati wa mchana kama sio lazima. Ikiwa ni lazima kuzunguka, unafaa **kubeba vitambulisho vyako vya usajili** kila wakati. Zaidi, hakikisha unafwatilia maagizo yanayotolewa na serikali ya Kenya na hakikisha unayafuata.

Nambari za dharura za usaidizi

- ***Kwa usajili/dharura za vitambulisho:***
Sekretarieti ya masuala ya Wakimbizi Shauri Moyo: 0772057770
- ***Nambari ya msaada ya UNHCR:*** 0800720063 (bila malipo)
- ***Kwa dharura za kiafya:***
NCCK 0704873342 / 0723281352/ 0723281362
- ***Kwa dharura za kisheria (kukamatwa, shida na polisi):***
Kituo cha Sheria 0720806531
- ***Kwa dharura za riziki:***
Danish Refugee Council 0800720181
- ***Kwa masuala yanayohusiana na NHIF (Mfuko wa kitaifa wa bima ya hospitali):*** 0740049502

Ukiwa na **dalili zozote za COVID-19** kama homa, kikohozi, upungufu wa pumzi na shida ya kupumua, **tafadhali wasiliana na wizara ya afya** kupitia 0800721316 (bila malipo); 0732353535; or 0748592558 kwa mwongozo.